



**SÄTERS
KOMMUN**

Kujipima mwenye we Covid-19 Dalarna

Ikiwa kutakuwa na dalili za kuumwa, unapaswa kufanya hatua za kupatiwa nafasi ya kwenda kuchukuliwa sampuli. Unaweza kuwasilisha sampuli moja tu katika kipindi cha ugonjwa. Ni kwa watu wale tu walio na dalili za ugonjwa ndio wanapaswa kuwasilisha sampuli.

Kuwasilisha sampuli hakugharimu chochote.

Njia ya utekelezaji wa namna ya kuchukuliwa sampuli hutofautiana kulingana na umri.

Soma zaidi kwenye wavuti ya mkoa wa Dalarna: www.1177.se



Skana nambari ya QR yaani QR-koden kwa kutumia simu yako ya mkononi yaani mobili ili ufike kwenye wavuti yaani hemsidan.

Watu wazima pamoja na vijana kuanzia miaka 13

Unapaswa kufanya hatua za kupatiwa nafasi ya kuchukuliwa sampuli binafsi yaani kujipima mwenyewe Covid-19 huko Dalarna ikiwa haya yafuatayo yanakubaliana na hali yako.

- Unakuwa na dalili za ugonjwa huo angalau katika masaa 24.
- Wewe ni mtu anayeitwa mawasiliano ya kaya yaani mkaazi wa nyumba husika na umearifiwa kuwa utachukuliwa sampuli.
- Umeombwa na wafuatiliaji wa maambukizo kwamba unapaswa kuchukua sampuli.



SÄTERS KOMMUN

Unaweza ukachukua sampuli wewe mwenyewe binafsi katika pua na koo kwa kutumia ka-fimbo/kjiti maalumu cha kuchukulia sampuli. Wazazi/Walezi wanapaswa kuwasaidi vijana walio chini ya umri wa miaka 16 wakati wa kuchukua hiyo sampuli.

Unaingia katika 1177 Mwongozo wa huduma ya afya yaani 1177 Vårdguidens yenye huduma za kielektroniki yaani e-tjänster kwa kutumia pamoja na Mobilt BankID, BankID, Freja e-id plus au kitambulisho kingine. Unapaswa kuchagua wewe mwenyewe eneo la kuchukuliwa hiyo sampuli na muda yaani saa.

Watoto kutoka miaka 10 hadi na ikiwa ni pamoja na miaka 12

Mzazi au Mlezi mwingine wa mtoto anashauriwa kufanya hatua za kupatiwa nafasi ya kuchukuliwa sampuli binafsi yaani kujipima mwenyewe kama:

- Mtoto anakuwa na dalili za ugonjwa wa Covid-19
-
- Mtoto alishakuwa na dalili za ugonjwa huo angalau katika masaa 24
-
- Mtoto ni mtu anayelitwa mawasiliano ya kaya yaani mkaazi wa nyumba husika na amearifiwa kuwa atachukuliwa sampuli
-
- Mtoto ameombwa kwa kusesitizwa na wafuataliaji wa maambukizo kwamba anapaswa kuchukua sampuli.

Mzazi/Mlezi anapaswa kumsaidia mtoto kwa ajili ya kuchukuliwa sampuli. Mzazi au Mlezi mwingine anatakiwa kuingia katika 1177 Mwongozo wa huduma ya afya yaani 1177 Vårdguidens yenye huduma za kielektroniki yaani e-tjänster pamoja na kuagiza kuchukua sampuli yaani vipimo kwa kupitia wawakilishi/wakala, na msaidie mtoto kufanya vipimo hivyo.

Watoto kutoka darasa la mapema hadi na ikiwa ni pamoja wenye umri wa miaka 9

Mzazi au Mlezi mwingine anashauriwa kupata nafasi ya muda wa kuchukuliwa kipimo cha sampuli toka mtoto, ambapo tendo hilo hufanywa na wauguzi wa kituo cha afya.

Mzazi au mlezi mwingine anapaswa kupiga simu kwenye kituo cha huduma za afya pamoja na kushughulika na kupata nafasi ya kufanya hatua za kufanya vipimo vya sampuli.